


YOTE NI KUHUSU

UHUSIANO



**KUYAREJESHA
MAHUSIANO YETU
YALIYOVUNJIKA**

YOTE NI KUHUSU UHUSIANO

Kukabiliana na udhaifu wetu.

Tunaishi katika ulimwengu wenye mahusiano yaliyovunjika. Watu wengi huwatumia wenzao kwa matamano yao wenyewe. Wanapoitimiza haja yao, au wanapohisi kuwa wamepata ‘mpango mwema zaidi’, wanawatupilia mbali au kuwaacha.

Wachache tu ni waaminifu kwa viapo walivyovifanya wao wenyewe. Kama watu waliovunjika, huwa tunaangazia ‘mimi’.

Je, unaye, au unamjua yeyote anayekumbana na mojawapo ya yafuatayo?

Vita	Biashara ya binadamu	Mauaji
Dhulma za kimapenzi	Ndoa zilizo vunjika	Kutoaminika
Machafuko	Umaskini	Magenge
Kashfa za kifedha	Misukosuko ya kisiasa	Kesi
Ubaguzi wa rangi	Jamii zinazoumia	Ufisadi
Dhuluma kwa watoto	Ubakaji	Chuki
Wizi wa mabavu	Ulevi	Mateso



BAADHI WANGEPENDEKEZA KUWA SULUHISHO LA MATATIZO HAYA NI:

Polisi wengi zaidi, Wanasiasa, majela, sheria, wanasheria, Mahakimu, dini, elimu au pesa....

Shida yetu kuu sio ya kisheria, kifedha, kidini, kimawazo au kielimu. Tunazo shida katika mahusiano na kiini chake ki mioyoni yetu

“Moyo ni mdanganyifu kuvipita viungo vingine vyote, na wala hauna tiba..” Jeremiah 17:9

Tunauhitaji moyo mpya.

“Nitawapa moyo mpya na kisha niweke roho mpya ndani yenu .” Ezekieli 36:26

Upendo wa kustaajabisha wa Mungu unaweza kutuumbia moyo mpya ndani yetu. Na tutazame:

MUHTASARI WA MAWASILISHO MANNE MAKUU

1. Umuhimu wa, na gharama ya uhusiano ulioimarishwa .
2. Jinsi uhusiano ulioimarishwa unavyokaa.
3. Tunayofanya ili kuurejesha uhusiano wetu na Yesu.
4. Baadhi ya matokeo ya kipekee ya uhusiano uliorejeshwa.



© John Hendee & Jim Phillips, 2016

All rights reserved.

Unless otherwise noted all scripture references are from the New International Version © 1973, 1978, 1984 by International Bible Society.

YOTE NI KUHUSU UHUSIANO

KIPINDI CHA KWANZA

UMUHIMU WA, NA GHARAMA YA UHUSIANO
ULIOREJESHA



UMUHIMU WA UHUSIANO ULIOREJESHWA

MTU

Njia zote za mtu
huonekana nzuri kwake.

Methali 16:2

BIBILIA INASEMA KWAMBA...

HATUKO WAKAMILIFU “Hakuna aliye mwema hata mmoja, kwa kuwa wote wametenda dhambi na kupungukiwa na nehemu ya Mungu” *Warumi 3:10, 23*

MATOKEO: Kwa kuwa mshahara wa dhambi ni mauti...” *Warumi 6:23*

TUMEZIVUNJA AMRI ZA MUNGU “Mwalimu, katika sheria zote, ni ipi iliyo kuu zaidi?

Yesu akajibu: Mpende Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote, kwa roho yako yote na kwa akili yako yote.’Na ya pili ni kama hiyo: ‘Mpende jirani yako kama jinsi unavyojipenda wewe.” *Mathayo 22:36-39*

MATOKEO: “Wote ambao hutegemea kutii sharia, wako chini ya laana”. *Wagalatia 3:10*

TU VIPOFU

“mungu wa enzi hizi amewafumba macho ya wasioamini, ili wasipate kuuona mwanga wa injili...” *II Wakorintho 4:4*

MATOKEO: “...Hajui anakoenda kwa kuwa giza nilempofusha.” *I Yohana 2:11*

TUMEPOTEA NJIA

“Wao huenda mbali na aliko Mungu.” *Waefeso 4:18*

MATOKEO: “Ipo njia ionekanyo nzuri machoni pa mwanadamu, ila mwishowe, humwelekeza kwenye mauti.” *Methali 14:12*

TUMEKUFA KIROHO “Nanyi mlikuwa mmekufa ndani ya dhambi na uovu wenu ...”

Waefeso 2:1

MATOKEO: “Nao sharti watoe habari zao katika hukumu mbele zake aliye tayari kuwahukumu walio hai na waliokufa.” *I Petro 4:5*

HATUWEZI KUJIOKOA “Mitume walistaajabika zaidi na kusemezana ‘Ni nani basi, anayeweza kuokolewa?’ Yesu aliwatazama na kuwajibu, kwake mwanadamu, hilo haliwezekani.” *Mariko 10:26-27*

MATOKEO: “Kumbukeni mlipokuwa mmetenganishwa na Kristo bila tumaini wala Mungu ulimwenguni” *Waefeso 2:12*

MUNGU

BIBILIA INASEMA KUWA...

MUNGU NI MKAMILIFU NA MTAKATIFU

“Njia zako, Ewe Mungu, ni takatifu. Ni mungu mwingine yupi mkuu kumshinda Mungu wetu?” *Zaburi 77:13*

MUNGU NDIYE HUPEANA AMRI

“Kuna mmoja pekee apeanaye amri, ambaye pia ni hakimu...” *James 4:12*

YESU NI NURU

“...Mimi Ndiye nuru ya ulimwengu ...” *Yohana 8:12*

YESU NDIYE NJIA

“Yesu akajibu, ‘Mimi ndiye njia, ukweli na uzima. Hakuna ajaye kwa Baba ila kwa njia yangu mimi” *Yohana 14:6*

YESU NDIYE CHANZO CHA UZIMA

“Kila atakayeisikia sauti yangu na kumwamini aliyenituma. Yeye amevuka kutoka kwa mauti na kuingia kwenye uzima.” *Yohana 5:24*

YESU NDIYE CHANZO CHA MSAADA WETU

“Yesu Aliwatazama, kisha akasema, ‘Kwa mwanadamu, hili haliwezekani, ila kwake Mungu, yote yanawezekana.” *Mariko 10:27*



Hatuwezi kuurejesha uhusiano wetu na Mungu kwa kuwa wema, kutenda mema au kuwa wa dini au makanisa ya ukweli. Hatuwezi kujiokoa.

Isaya 64:6 inasema:

“Wema wetu wote ni kama matambara machafu.”

Mpango wa Mungu sio kutupea sisi haki yetu, bali ni kutulinda dhidi ya hukumu ya haki.


Hiyo inaitwa Rehema yake Mungu.

GHARAMA YA UHUSIANO ULIOREJESHA

“MUNGU AMEKUJA KUWASAIKIA WATU WAKE.” LUKA 7:16

“Kwa kuwa yeye hutamani kuokolewa na kuelewa ukweli huu: kuwa Mungu yumo upande mmoja, nao watu wote upande wa pili, naye Yesu Kristo, yeye akiwa kama mwanadamu yuasimama kati kati kuwapatanisha kwa kuutoa uhai wake kwa wanadamu wote.”

I Timotheo 2:4-6 (LB)



UPENDO WA MUNGU SI WA KAWAIDA!

“Na mkawe na uwezo wa kuelewa, kama watu wote wa Mungu wanavyopaswa, upana, urefu, na kimo cha upendo wake vilivyo. Na mkaupate upendo wa Kristo ingawaje ni mkuu kiasi kuwa hauwezi kueleweka wote. Na hapo mkawe wakamilifu kwa uzima wote na nguvu ambazo hutoka kwa Mungu.” Waefeso 3:18-19

Kuipata dhamana hii ya nehema humfanya maskini hohehahe kuwa mwana wa mfalme; kuikosa zawadi hii humfanya aliye tajiri wa wote kuwa omba-omba.

-Max Lucado

YOTE NI KUHUSU UHUSIANO KIPINDI CHA PILI

Jinsi Uhusiano Uliorejeshwa Unavyoonekana.



Jinsi Uhusiano Uliorejeshwa Unavyoonekana

Bibilia ni hadithi ya jinsi Mungu anavyoimarisha uhusiano wa upendo na mwanadamu.

Mungu hujidhihirisha kwetu sisi na kutupa upendo na uzima kupitia kwa agano.

Ukurasa huu unaielezea taswira yote, maudhui na hadithi nzima ya Bibilia.

Mkataba: agano, makubaliano, wosia, muungano.

Mkataba huwa na angaa sehemu nne:

Wahusika—Wale wanao ingia kwenye makubaliano: Mungu na mwanadamu.

Masharti—Yale mwanadamu anakubali kumfanyia mungu.

Ahadi—Yale Mugu anamwahidi mwanadamu.

Matokeo—Matokeo ya kutotimiza au kukataa mkataba na Mungu..

Bibilia ni historia ya mikataba iliyofanywa na Mungu kwake mwanadamu. Ni tofauti na kandarasi. Kandarasi huwa na ubinafsi na hujikinga mmoja kutokana na mwingine. Mkataba ni makubaliano ambapo pande zote mbili hukubali kuyatekeleza kwa dhati yale yanayomnufaisha yule mwingine; hauna ubinafsi.

Tangu kabla ya uumbaji, Mungu alimpangia msamaha na uzima wa milele mwanadamu.

“...imani ni uhakika wa uzima wa milele, ambao mungu asiyedanganya aliahidi tangu mwanzo wa nyakati. .” Tito1:2

Mungu aliidhihirisha nia na upendo kupitia kwa makubaliano kadhaa. Katika roketi, kapsuli ndiyo sehemu muhimu zaidi:

Tuanzie chini kwa # 1 kisha tukienda juu:

5-Kisha aliufanya mkataba mwema zaidi na sisi kupitia kifo cha mwanaye. Wahibrania 8:6

4-Alifanya mkataba na Israeli.

(Uzao wa Ibrahimu) Kutoka 19:5

3-Alifanya mkataba na Ibrahimu..

Mwanzo15:18

2-Alifanya mikataba miwili na Nuhu.

Mwanzo6:18 & Mwanzo 9:9,11

1-Mungu alifanya mkataba na Adamu. Hosea 6:7



Mikataba ya Mungu inadhahirisha kuwa Mungu ni mwaminifu na daima huzitimiza ahadi zake.

“ Kwa kuwa lote lililoandikwa liliandikwa ili kutufunza, ndipo kupitia uvumilivu na kushawishiwa na Bibilia, sisi tupate imani.” Waroma 15:4

Mikataba yote ya Mungu huelekeza katika Agano Jipya: zawadi na dhamani.

AGANO JIPYA

Agano jipya lilianza pale ambapo Yesu alikufa na kumwaga damu yake msalabani:

“Kristo ndiye mpatanishi wa Agano Jipya, kwamba wale walioitwa, waupokee uridhi wa milele ulioahidiwa kwa kuwa yeye ameshakufa kama kafara na kuwaweka huru.”

Wahibrania 9:15

Agano jipya ni bora kuliko lile la zamani. Nayo huduma aliyoipokea Yesu ni ya kiwango cha juu kuliko yao, kama vile agano ambalo Yeye ndiye mpatanishi lilivyo bora kuliko lile la zamani, na ahadi zake pia ni bora.” Waibrania 8:6

Ni kuhusu uhusiano

Mwaliko wake:

“Njooi kwangu enyi nyote mliolemewa na mizigo, nami nitawapa pumziko. Utwaeni mzigo wangu kwenu nyinyi na mjifunze nami , kwa kuwa mimi ni mpole wa moyo, na mtapata pumziko kwa roho zenu.” Mathayo11:28, 29

“Sasa tunaufurahia uhusiano wetu wa kiajabu na Mungu- yote kutokana na lile Yesu Kristo Bwana wetu alivyofanya kwa kutufia kwa minajili ya dhambi zetu, na kutufanya marafiki wa Mungu.” Waroma 5:11LB

Zamani kabla yako wewe uamue utakavyofanya na Mungu, Mungu alikuwa ameshaamua atakalofanya nawe.

-Louie Giglio

Agano Jipya La Mungu

“Awali, Mungu aliamua kutuleta sisi kwa familia yake yeye kwa kutuleta kwake kupitia kwa Yesu Kristo.” Waefeso 1:5 TLB

Mungu anataka sisi tuwe na uhusiano mwema naye na hata wenzetu.

WAHUSIKA KATIKA AGANO JIPYA

Mungu na yeyote aingiaye ndani ya Kristo. Imepaanwa kwa watu wote; wa rangi, viwango, mataifa yote, kwa walevi, wazinifu, wauaji, wafungwa, walioshindwa, washindi, wa dini na hata wasio wa dini. Wote wamealikwa.

AHADI ZA MUNGU hutufanya watu wapya. “Kwa hivyo, iwapo yeyote yumo ndani ya Kristo, yeye ni kiumbe kipya, ya kale yameisha na mapya yamewadia.” 2 Wakorintho 5:17 LB.

Ahadi za Mungu...

Upendo—Yohana 3:16 & Warumi 8:38-39

Kutohukumwiwa—Wakolosai 1:22

Msamaha—Matendo 2:38

Dhambi zetu kusahuliwa—Wahibrania 8:12

Ufufuo—I Wakorintho 6:14 & 15:51-53

Uzima wa Milele—I Yohana 5:11 & Warumi 6:23

Kuishi pamoja na Mungu Milele—Ufunuo 21:1-4

Maisha yaliyokamilika—Yohana 10:10

Furaha—I Petero 1:8

Kuzaliwa upya—Yohana 3:3,7

Kufanywa Wana—Waefeso 1:5 & Warumi 8:15

Familia—Wagalatia 6:10

Uwepo—Mathayo 28:20

Msaada wa kila siku—Warumi 8:26-28 & Wafilipi 1:6

Utulivu wa ki-akili—Waefeso 4:23-24

Mwelekeo—Waefeso 2:10

Uraia—Wafilipi 3:20

Roho ndani yetu—I Wakorintho 3:16 & Warumi 5:10, 8:9

Mamlaka ya kuishi—Waefeso 3:21

Usalama—2 Petero 3:17

Ushindi mkuu—I Yohanan 5:4-5 & Warumi 8:37

Kuteswa—II Timotheo 3:12

Shinikizo—II Wakorintho 5:13-14

Kuteseka—I Petero 1:6

Imani—II Wakorintho 1:10b

Kupenda nidhamu—Ufunuo 3:19

Kuelewa—Wahibrania 4:15

Uridhi—I Petero 1:4

Ukaribu na Kujiamini—Wahibrania 4:16

Mungu HATUAHIDI UTAJIRI WA MALI, Mungu HATUAHIDI utajiri wa mali, afya njema, kazi, au kuepuka matatizo na mateso.

Mungu hutuahidi nguvu za kustahamili.

Nimewaambia mambo haya ndipo kupitia kwangu mimi, nyinyi mpate kuwa na amani. Hapa duniani, ni lazima uwe na shida. Lakini jipe moyo! Mimi nimeushinda ulimwengu!
”Yohana 16:33

Mungu anatahidi amani yake.

Kwa kuwa tumetakaswa mbele za Mungu na ahadi zake, tunaweza kuwa na amani ya kweli kwa yale Yesu Kristo Bwana wetu ametufanyia.” Warumi 5:1 LB

MASHARTI YA MWANADAMU

Ninayokubali kumfanyia Mungu

Kwanza: “Mpende Bwana Mungu wako kwa roho yako yote, kwa moyo wako wote na kwa akili yako yote. Hii ndiyo amri ya kwanza na ya umuhimu zaidi..” Mathayo 22: 37,38

Pili: “Na ya pili ni hii, ‘Mpende jirani yako kama jinsi unavyojipenda wewe.’” Mathayo 22:39

Yote yaliyoandikwa katika Agano Jipya linakusudiwa kutufundisha jinsi ya kuyafanya mambo haya.

Yesu alitunyeshwa jinsi ya kumpenda binadamu na Mungu (Warumi 8:29). Aliwapenda wazuri, wabaya, waliokataliwa, wapweke, wasiotii, waliohamishwa, waliotelekezwa na wasio wema.

Kwa kuwa upendo wa Kristo hutushinikiza kwani tunaamini kuwa mmoja alitufia, kwa hivyo wote walikufa. Na aliwafia wote, ili wale wanaoishi wasiishi tena kwa ajili yao wenyewe ila kwa ajili yake yeye aliyewafia na akafufuka. Haya yote yanatokana na Mungu aliyetupatanisha tena na yeye mwenyewe kupitia kwa Kristo na akatupatia huduma ya upatanishi: 19 kuwa Mungu alikuwa anjipatanisha na ulimwengu pasi na kuzihesabu dhambi za wanadamu dhidi yake. Na ametuhakikishia sisi habari ya upatanishi. Sisi basi ni mabalozi wa Kristo, kama kwamba Mungu anatoa mwito kupitia kwetu sisi. Tunakusihia kwa niaba ya Kristo: Patanishwa na Mungu.. 2 Wakorintho 5:14-15 & 18-20

Kupenda kama Kristo alivyopenda, na kuishiriki hadithi yake ndilo shinikizo kuu la maisha yangu mapya.

Yesu ndiye Zawadi kuu zaidi kutoka kwa Mungu

“Kwake tunao ukombozi kupitia kwa damu yake, msamaha wa dhambi, sawa na wingi wa nehema zake alizotupa sisi. Na hekima yote...” Waefeso 1:7-8

YOTE NI MAPYA...

Upendo – “Kwa jinsi Mungu alivyopenda ulimwengu hata akamtoa mwanawe wa kipekee, ili yeyote amwaminiye asipotee ila apate uzima wa milele”. Yohana 3:16

“Kwa kuwa ninayo imani kuwa sio mauti wala uzima, malaika wala mizimu, wakati huu au ujao, wala nguvu zozote, sio urefu wala kina, wala chochote kilichoumbwa kinachoweza kututenganisha na upendo wa Mungu ulio ndani ya Yesu Kristo, Bwana wetu”. Warumi 8:38-39

Kutohukumiwa – Ila sasa amewapatanisha kwa mwili wa Kristo kupitia kifo na kuwatakasa machoni mwake, pasiwe na doa na huru kutokana na hukumu. Wakolosai 1:22

Msamaha – Petero akajibu, “Tubuni na mbatizwe, kila mmoja wenu, kwa jina la Yesu Kristo kwa msamaha wa dhambi zenu.” Matendo 2:38—Mwenye kusamehewa.

Hatazikumbuka dhambi zetu – “Kwa kuwa nitawasamehe maovu yao na wala sitazikumbuka dhambi zao kamwe.” Waibrania 8:12

Ufufuo – Kwa uwezo wake, Mungu alimfufua Bwana wetu kutokana na mauti, na atatufufua na sisi pia. I Wakorintho 6:14

Sikilizeni, nawaambieni fumbo: sisi wote hatutalala, ila tutabadilishwa- mara moja katika kufumba jicho, katika tarumbeta ya mwisho. Kwa kuwa, tarumbeta italia na wafu watafufuliwa, pasi na madhara yoyote, na tutabadilishwa. Kwa kuwa wa kuisha atajisitiri na cha kuisha naye wa kuishi, kwa uzima wa milele.

I Wakorintho 15:51-53

Uzima wa milele – “Na huu ni ushuhuda: Mungu ametupa uzima wa milele na uzima huu upo ndani ya mwanawe”. I Yohana 5:11

“Kwa kuwa mshahara wa dhambi ni mauti, ila zawadi ya Mungu ni uzima wa milele ndani ya Yesu Bwana wetu.” Warumi 6:23

Pamoja na Mungu Milele – “Kisha nikaona ‘mbingu mpya na nchi mpya’, kwa kuwa mbingu

ya kwanza na nchi ya kwanza zilikuwa zimepita,



na wala hapakuwa tena na ziwa lolote. Niliuona mji mtakatifu, Yerusalemu mpya, ukishuka kutoka mbinguni kwa Mungu kwa mapambo kama vile bibi harusi anavyopambwa kwa ajili ya mumewe. Kisha nikaisikia sauti kuu kutoka kwa enzi ikisema, “Tazama! Makao ya Mungu sasa yamo kwa wanadamu, naye ataishi nao. Watakuwa watu wake naye atakuwa Mungu wao. ‘Atalipanguza kila chozi la macho yao. Hakutakuwa tena na kifo’ wala kuomboleza, kilio wala machungu, kwa kuwa ya kale yamepita”. Ufunuo 21:1-4

Uzima tele – “Mwizi huja tu kuiba, kuu na kuharibu. Nimekuja ili wawe na uzima, uzima tele”. Yohana 10:10

Furaha – “Ingawaje hamjamwona, mnampenda na hata ingawa hammuoni sasa hivi, mnamuamini na mmejawa na furaha isiyoelezeka”. I Petero 1:8

Kuzaliwa Upya - Yesu akajibu, “Kwa kweli nawaambieni, hakuna atakayeona ufalme wa Mungu mpaka azaliwe mara ya pili. Yohana 3:3

Hamfai kushangazwa ninaposema “lazima mzaliwe mara ya pili.” Yohana 3:7

Kwa kuwa mmezaliwa mara ya pili, sio kwa mbegu iharibikayo, ila ya kudumu, kupitia kwa kudumisha neno la Mungu katika maisha yenu.

I Petero 1:23

Kufanywa wana – “Roho mliyoipokea haiwafanyi kuwa watumwa ili muishi kwa hofu tena; bali, roho mliyoipokea ilileta kutwaliwa kwenu na kuwa wana. Na kupitia kwake sisi hulia “Abba, Baba.” Warumi 8:15

Jamii – “Kwa hivyo, kila tunapo na nafasi, tuwatendee wema watu wote, hasa wale wa jamii ya wanaoamini”. Wagalatia 6:10

Uwepo— “Na hakika, mimi niko pamoja nanyi wakati wote hadi mwisho wa nyakati”. Mathayo 28:20b

Msaada wa kila siku – “Kwa njia hiyo hiyo, Roho hutusaidia katika unyonge wetu. Hatukijui kinachopasa tuombe kwa ajili yake, lakini Roho hutuwakilisha kupitia sauti zisizokuwa maneno. Naye ambaye huisaka mioyo yetu anaifahamu akili ya Roho kwa kuwa Roho huomba kwa niaba ya watu wa Mungu kulingana na mapenzi ya Mungu. Na tunafahamu kuwa katika mambo yote, Mungu hutenda mema kwa wale wanaompenda na walioitwa kwa mapenzi yake”. Warumi 8:26-28

Mawazo dhana – “Mfanywe wapya katika dhana za mawazo yenu; na mjitwike uwepo upya, kama mlivyoumbwa kuwa kama Mungu kwa wema na utakatifu”. Waefeso 4:23-24

Mpango – “Kwa kuwa sisi ni kazi ya mikono ya Mungu, tulioumbwa kwa Kristo Yesu kutenda mema ambayo mwanzoni, Mungu alikusudia tuyafanye”. Waefeso 2:10

Uraia – “Uraia wetu ni wa mbinguni. Na tunamngoja mwokozi kutoka huko, Bwana Yesu Kristo”. Wafilipi 3:20

Roho ndani yetu – “Je, mnafahamu kuwa nyinyi ni hekalu ya Mungu na kuwa Roho wa Mungu huishi ndani yenu?” I Wakorintho 3:16

Mamlaka ya kuishi – “...Utukufu wote kanisani na uwe wake yeye kupitia kwa Kristo na uenee kwa uzao wote milele! Amina.” Waefeso 3:21

Usalama—“Kwa kuwa tayari mnayafahamu haya, kaeni macho msije mkahadaiwa na uovu wa mwanadamu na kuanguka kutoka nafasi yenu.”

II Petero 3:17

Ushindi Mkuu - Kwa kuwa kila aliye wa uzao wa Mungu huushinda ulimwengu. Na huu ndio ushindi uliushinda ulimwengu- imani yetu. Ni nani yeye ambaye huushinda ulimwengu? Ni yule tu anayeamini kuwa Yesu Kristo ni Mwana wa Mungu. I Yohana 5:4-5

Kuteswa— Bila shaka, yeyote anayetaka kuishi maisha ya ki-Ungu sharti atateswa... II Timotheo 3:12

Shinikizo— Kwa kuwa Upendo wa Kristo hutushinikiza. II Wakorintho 5:14

Kuteseka—Furahini katika kuteseka kwenu, kwa kuwa ni muda mfupi tu mtakapoyapitia majonzi na majaribu ya aina zote. I Petero 1:6

Tumaini—Kwake yeye tumeweka tumaini letu kuwa, yeye atazidi kutukomboa. II Wakorintho 1:10b

Kupenda nidhamu— “Wale mimi ninaowapenda, huwakemea na kuwaadhibu. Hivyo, kuweni wastahamilifu na mtubu”. Ufunuo 3:19

Kuelewa— “kuwa hatuna kuhani mkuu asiyetuhurumia katika unyonge wetu, ila tunaye yeye ambaye ameshajaribiwa kwa njia zote, kama sisi, wala yeye hakuwa na dhambi”. Wahibrania 4:15

Uridhi – “Na huko mbinguni, mmewekewa nyinyi uridhi ambao kamwe hauta haribika au kuisha”. I Petero 1:4


Ukaribu na kujiamini – “Kwa hivyo, natuelekee kwa ushujaa kwenye enzi ya Mungu wetu wa rehema. Hapo tutaipokea rehema yake ya kutusaidia tunapoihitaji zaidi”.

Wahibrania 4:16

**YOTE NI KUHUSU
UHUSIANO**

KIPINDI CHA TATU

**TUNAVYOPASWA KUFANYA ILI KUUREJESHA UHUSIANO
WETU NA YESU**



JINSI YA KUUREJESHA UHUSIANO WETU NA MUNGU

Uhusiano mpya na Mungu huanzia katika kumwamini.

“Kwa jinsi Mungu alivyopenda ulimwengu kisha akamtoa mwanawe wa pekee ili yeyote amwaminiye asipotee, bali aupate uzima wa milele .” Yohana 3:16

Imani kwake Mungu ni “kushawishika bila shaka yoyote kuwa Mungu anazo nguvu za kuyatekeleza yale yote aliyoyaahidi.” (Warumi 4:21).

“Basi tunaweza kujivunia nini ili tuupate wokovu? Hakuna lolote. Kwa nini? Kwa kuwa msamaha wetu si kwa matendo yetu mema : bali ni kutokana na matendo ya Kristo na imani yetu kwake.” Warumi 3:27

HII NI HABARI NJEMA!

Hatuwezi kufanya LOLOTE kumfanya Mungu atupende zaidi ya anavyotupenda.

Kujaribu kujiokoa au kuwa wema wa kutosha hutuchosha na kutufanya tufe moyo.

Imani ya ki Bibilia ni:

Kuamini (*Kwenye akili*) kuwa Mungu alikuwa Binadamu ndani ya Yesu , kwamba alikufa kwa dhambi zetu na kuwa alifufuka kutoka kwa kaburi. “Kwa kuwa yote niliyoyapokea niliwapa nanyi kama umuhimu zaidi: kuwa Yesu alikufa kwa ajili ya dhambi zetu kama maandiko yanavyosema kwamba alizikwa na akafufuka siku ya tatu kama maandiko yanavyosema.” I Wakorintho 15:3-4

Imani ya ki-Bibilia inahitaji hakika ya akili na mwitikio wetu.



Katika miaka ya sitini palikuwa na mvukia kamba mashuhuri aliyetitwa Blondin. Aliizuru nchi yote akifanya maonyesho. Hatimaye alifika Niagara Falls kuanza onyesho lake la siku tatu. Blondin aliuvuta ukamba wake juu ya Niagara Falls, na kwa siku mbili, akawa anaupitia, huku akiwavutia watazamaji wengi. Siku ya tatu, akasema kuwa, angetembea juu ya ukamba ule akiwa amefunikwa uso na tena akilisukuma toroli. Lakini kwanza akawaendea watazamaji na kuwauliza iwapo waliamini kuwa angeweza kulitenda jambo lile. Na katika umati ule wote, hakuna ambaye hakuamini. Hapo basi aliporudi kwenye ukamba, aliwauliza mmoja wao ajitolee na

“Kwa njia sawa na hiyo, imani tu, isipoandamana na matendo, imekufa.” James 2:17

Tumaini huleta imani na upendo.

“Imani na upendo ambazo hutoka kwa tumaini.” Wakolosai 1:5

Imani huleta Kumpenda Mungu.

“Nijapokuwa na imani, hata ya kuiamrisha milima, kama sinao upendo, mimi si kitu kabisa.” I Wakorintho 13:2b

Tunahitaji kuwa na mizizi yetu ndani ya upendo.

“...Ninamuomba Kristo aishi ndani ya roho zenu kwa imanina ninaomba kuwa nyinyi mpate kukita mizizi ndani ya Upendo.” Waefeso 3:16-17

Imani na upendo huleta utiifu.

Upendo wa Ukweli huleta Toba

“Mwanzoni, Mungu alisamehe kutojua kama huku, lakini wakati huu anawaamrisha watu wote watubu.” Matendo 17:30

Katika Matendo 2:14 tunalisoma funzo la kwanza la Petero kwa watu wasioamini baada ya kufa kuzikwa na kufufuka kwa Yesu.

Petero alivyobaini:

“Basi na Waisiraeli wote waamini hivi: Kuwa Mungu alimuumba Yesu mliomsulubisha, yeye aliye Bwana, na Kristo.” Matendo 2:36

Hapa Tunasoma majibu ya watu:

“Maneno haya ya Petero yaliwashangaza sana, nao wakamwuliza pamoja na watume wengine, “Tutafanya nini?”” Matendo 2:37b

Kuuliza huku kuliashiria kuwa WALIAMINI habari hiyo. Imani yao mpya ilihitaji kitendo fulani.


Jibu la Petero

“Petero akajibu, Tubuni na mbatizwe, kila mmoja wenu, katika jina la Yesu Kristo ili mpate msamaha wa dhambi zenu. Nanyi mtapata Zawadi ya Roho Mtakatifu.” Matendo 2:38

Toba inamaanisha ‘kugeuka’

Toba ya kidini ni kujaribu kuandika mambo yanayokufaa kufanya na yale usiyofaa kuyafanya ili kukubaliwa na Mungu, na hivyo, kuokolewa.

Toba ya ki Kristo ni kugeuka kutoka kumkataa Yesu na kumwamini - ni kuhusu kumrudia na kuurejesha uhusiano naye.



Akitumia mfano, Yesu alisema kuwa hatuwezi kuwatumikia mabwana wawili. Tunapotubu, tunasema kuwa, ‘atakuwa Yesu’.

Katika macho ya Mungu, aidha tunamtumikia yeye, au Shetani. Shetani anataka tumtumikie yeye na kuuharibu uhusiano wetu na Mungu.

“Watakao mpinga, yeye ata waamrisha kwa upole, kwa imani kuwa Mungu atawapa toba, na wapate kuujua ukweli, wajirudi na kasha wamtoroke shetani aliyewashika mateka ili wamtumikie.” II Timotheo 2:25-26

“Je, huoni uajabu wa nehema fadhili na upole wake Mungu alio nao juu yako? Hili halina maana yoyote kwako wewe? Je, huoni kuwa nehema yake imekusudiwa kukuondoa wewe kutoka kwa dhambi zako?” Warumi 2:4

“Tubuni basi, na mmrudie Mungu, ndipo dhambi zenu ziondolewe, ndio mida ya pumzisho iwajieni nyinyi kutoka kwa Bwana.” Matendo 3:19

Upendo wa Mungu kwetu, hutuletea imani ndani yake, kumpenda, kutubu, na kisha...

Kukiri ni mwitikio wangu wa maneno na kukubali uhusiano wangu na Yesu.

“Unapokiri na kinywa chako, kuwa ‘Yesu ni Bwana’ na unapoamini kwa moyo wako kuwa Mungu alimfufua kutoka mautini, utaokolewa.” Warumi 10:9-10

Kukiri ni kuzungumza upendo wangu kwa Yesu- ni imani yangu kwa vitendo

Fikiria mtu anayemposa mpendwa wake na kisha kuwaambia wengine hivi, “Jamani, ningependa kuwajulisha rafiki yangu.....”

Ubatizo ni amri ya Mungu ndani ya mwaliko wa agano lake

“Kisha Yesu akawajia na kuwaambia, ‘Nguvu zote za mbingu na nchi nimepewa mimi. Basi nendeni mataifa yote mkiwafanya wote wafuasi wangu, mkiwabatiza katika jina la Baba, la Mwana na la Roho Mtakatifu, na mkiwafundisha kuyatii yale yote niliyowafunza nyinyi...” Mathayo 28:18-20

Petero aliipitisha amri ya Mungu:

“Petero akajibu, ‘Tubuni na mbatizwe kila mmoja wenu, katika jina la Yesu Kristo ili mkapate msamaha wa dhambi zenu, na mtapata zawadi ya Roho Mtakatifu.’ Matendo 2:38

Katika lugha ya Kigiriki ambapo kutoka kwake Agano jipya limetafsiriwa, neno ‘batiza’ linamaanisha ‘kutumbukiza’ au ‘kuzamisha’.

Mungu Aliamrisha Ubatizo kwa Yesu

Ni jambo la Kutii Agano

Bibilia inaonyesha kuwa wanafunzi wanaweza kubatizwa siku yoyote, katika maji yoyote, na mwanafunzi mwingine yeyote.

Tunabatizwa ndani yake Yesu, na wala sio dhehebu

Ubatizo wa kikristo ni kiapo chetu cha uaminifu na utiifu kwake Mungu.

“...Nayo maji haya ni ishara ya ubatizo ambao huwaokoa pia- sio kuondoa achafu kwa mwili bali ni kuapa kuwa na mawazo mema kumhusu Mungu. Hukuokoa kwa ufufuo wa Yesu Kristo.” I Petero 3:21

Kiapo cha kujitolea

Miongoni mwa wagiriki, neno kiapo lilitumika pia wakati watu wawili walipo ingia kwenye mapatano ya ki-biashara. Muuzaji alitoa pendekezo, naye mnunuzi alifikiria. Iwapo angelikubali, angesimama na kusema, “Naapa kuwa nitaishi kulingana na masharti ya mkataba huu.” Hili lilifanyika mbele ya shahidi, na kiapo hicho kilimalizia mkataba na kuufanya patanishi.

Tunapopewa habari za upendo wa Mungu, tunaweza kuzikubali au kuzikataa. Hakuna la tatu. Tunajibu ndiyo au la. Tukiamua kujibu ndio, tuna fuatilia mapatano kwa kubatizwa. Tunapomgeukia Yesu na kusema kuwa tunataka kuwa wanafunzi wake,



Mungu hutuuliza tuape. Tayari, Mungu ameshaapa. Aliapa pale msalabani na akapiga sahihi kwa damu yake.

Vifungu vifuatavyo vinatufunza yale yanayotendeka katika ubatizo:

“...Enyi nyote mliobatizwa ndani ya Kristo, mmevalishwa na Kristo.” Wagalatia 3:27

“Na sasa unangoja nini? Simama, batizwa, na dhambi zako ziondolewe, unapoliita jina Lake.” Matendo 22:16

Tunajifia sisi wenyewe, ila yeye hujipeana kwetu sisi.



“Au, kwani hamjui kuwa enyi nyote mliobatizwa ndani ya Kristo, mliobatizwa kwa kifo chake? Basi, sisi tulizikwa pamoja naye, kupitia ubatizo huo, ili, kama jinsi Kristo yeye alivyofufuka kutoka kwa mauti kwa utukufu wa Mungu Baba, sisi pia tunaweza kuishi maisha mapya.” Warumi 6:3-4

Katika ubatizo, Paulo anasema, tunakumbana na mauti, kuzikwa na ufufuo wa Yesu.

AGANO LA NDOA HUTUSAIDIA KULIELEWA VYEMA AGANO NA KRISTO

Ndoa ni uhusiano wa ki-agano. Malachi 2:14

AGANO NDANI YA NDOA

Uhusiano huu huanza kwa imani maalum na uhakika katika kusema, ‘Nimempata niliyekuwa nikimtafuta.’

Uhakika huu huleta...

Kumpenda mwezio kwa moyo wako wote. Kusema, ‘Napenda kuishi maisha yangu yote na wewe pekee.’

Upendo huu na imani huleta...

Mmoja kupendekeza ndoa na mwingine kukubali. Upendo wa dhati hujipeana kumtakia mema mwenzio kwa kuuweka ufanisi wake kabla ya wako wewe.

“Wewe kwanza, wewe tu”. Msako umeisha.”

Je, kunayo makubaliano mengine yanayohitaji kutupiliwa mbali?

Kuwaambia wengine kuhusu kauli iliyochukuliwa. Kujitolea.

Sherehe ya Harusi

- Mwisho na Mwanzo.
- Kuuacha upweke na kuanza maisha ya ushirikian Ni uhusiano wa kipekee.
- Kiapo cha uaminifu kwa mwenzia peke yake.

Sasa, tuone faida na majukumu ya maisha ya ndoa.

Hatuwezi kuketi tu!

Kina na hali ya uhusiano wako vitategemea jinsi wewe na mwenzio mtakavyofanya kazi ya kuukuza uhusiano wenu.

AGANO NA KRISTO

Agano hili huanza kwa imani na uhakika wa kusema “nimempata ninayemhitaji: ninaamini Yesu Kristo ni Mwana wa Mungu, kwamba alikuja kunifia kwa dhambi zangu”.

Imani hii hujibu kwa.....

Kumpenda Mungu kwa moyo wangu wote, roho yangu yote na akili yangu yote.

Kwa upendo, najipeana kwa Yesu Kristo, na kuaahidi kumwamini na kumtii. Naziweka haja zake kabla ya zangu, kama yeye alivyonifanyia. Naukubali mwaliiko /pendekezo lake. Namweka Mungu katika enzi ya maisha yangu.

Wewe kwanza, wewe pekee. Msako umeisha= kutubu.

Je, kunayo mahusiano mengine yanayohitaji kutupitiwa mbali?

Kuwaambia wengine kuhusu kauli niliyoichukua: **Kukiri**

Ubatizo kwa Yesu, ni kile ambacho ni harusi katika uhusiano wa ndoa.

- Mwanzo na mwisho.
- Kutupilia maisha ya ‘upekee’ na kuingilia maisha ya ushirika
- Kupeana kiapo cha uaminifu.

Sasa ninaweza kuzifurahia ahadi za uhusiano wangu mpya na kuishi kuyatimiza masharti ya agano langu na Yesu..

Siwezi kuketi tu, na kutofanya lolote!

Kina na hali ya uhusiano wangu na Kristo vitaashiria jinsi ninavyofanyia kazi uhusiano wangu naye. Mungu atakuwa mwaminifu.

Je, uko wapi wewe katika Agano Jipya?

Hebu tuone...

**YOTE NI KUHUSU
UHUSIANO**

KIPINDI CHA NNE

**BAADHI YA MATOKEO YA KIPEKEE YA UHUSIANO NA YESU
ULIOIMARISHWA**



MATOKEO YA KIPEKEE YA UHUSIANO WA KIPEKEE NA YESU

Maoni ya mtu mmoja kuhusu Mkristo:

“Mkristo ni mtu ambaye anazidi kuwa kile ambacho kwa macho ya Mungu, ashakuwa.” (Msemaji hajulikani)

Usemi mwingine kama huu unapatikana katika Biblia:

“...kwa kuwa, kupitia kwa kafara moja tu, yeye daima amewasafisha wale wanao fanywa watakatifu.” Wahibrania 10:14

Kuna nyenzo mbili za maisha ya kikristo zinazofanya kazi kwa wakati mmoja

Kwa sababu ya upendo alio nao kwetu, Mungu hutufanya sisi wakamilifu mbele zake, daima, kwa msimamo wetu:

Msimamo wetu ni:

MAHALI: “... Nasi tuko nadani yake, yeye aliye mkweli-hata katika mwanawe Yesu Kristo. Yeye ndiye Mungu wa Ukweli na Uzima wa Milele.” I Yohana 5:20

ZAWADI: “Kwa kuwa ni katika nehema mlioweza kupata wokovu kupitia kwa imani na wala sio kutokana nanyi nyinyi, ni zawadi kutoka kwa Mungu- wala sio bidii yenu ndiposa yeyote kati yenu asijigambe.” Waefeso 2:8-9

SOBADILIKA: “Ninawaandikia mambo haya enyi mnaoliamini jina la mwana wa Mungu ndipo mpate kufahamu kuwa mnao uzima wa milele.” I Yohana 5:13

WOTE SAWA: “Hakuna Kati yenu myahudi wala Msamaria, mtumwa wala aliye huru mume au mke, kwa kuwa nyinyi wote ni kimoja katika Yesu Kristo.” Wagalatia 3:28

MTU MPYA: “ Kwa hivyo, iwapo yeyote yumo ndani ya Kristo, yeye anakuwa kiumbe kipya; uzamani unatoweka, na upya unawadia!” II Wakorintho 5:17

NAFASI YETU YA KIROHO ndani ya Yesu inatoka na upendo ulio juu yetu. I Yohana 4:19 inasema, “Tunampenda kwa kuwa yeye alitupenda kwanza.” Alitupenda, akatujia, akafa na kufufuliwa kutoka kwa wafu na sasa anatumwa sisi kama wana wake wa kiume na wa kike. Tumependwa kwa kina. Kuwa na ufahamu wa kuwa jambo hili litayabadili maisha na mioyo. Yote ni kuhusu Uhusiano.

Tunapokuwa ndani ya Yesu, Mungu kwa upendo hufanya kazi ya kuibadilisha hali yetu:

HALI Yetu NI:

SAFARI: Kuwa na uhakika huu; kwamba yeye aliye ianzisha kazi njema ndani yako, yeye huyo ataitimiza hadi siku ya Kristo Yesu. Wafilipi 1:6

Mungu anafanya kazi ya kutubadilisha.

KAZI INAYOENDELEA: “ Msiwe na lolote na hekaya zisizo na uungu ndani yake, wala zile za wake wakongwe:, ila mjifunze kuwa na uungu ndani yenu. Kwa kuwa mafunzo ya kimwili ni ya dhamana fulani, lakini uungu una dhamani kwa kila kitu, kwa kuzingatia ahadi katika uhai huu na uhai ujao.” I Timotheo 4:7-8

Inatufaa tushirikiane katika kazi hii ya mabadiliko.

KUBADILIKA: “Nasi tunabadilishwa na kupata uwepo kama wake na utukufu zaidi ambao hutokana na ambaye ni Roho.” II Wakorintho 3:18


HAMTOSHANI: ...Ingawa kwa sasa mnapaswa kuwa walimu, nyinyi wenyewe mnamhitaji mwalimu awafunze kwa mara nyingine. Mnahitaji maziwa na wala sio chakula kigumu! Yeyote aishiye kwa maziwa ni mtoto... Nacho chakula kigumu ni cha waliokomaa, ambao kwa uzoovu wa matumizi, wamejifunza tofauti kati ya mema na maovu. Wahebrania 5:12-14

MTAZAMO MPYA

Mlifundishwa kuhusu mienendo yenu ya awali, kutupilia mbali uwepo wenu wa awali ambao huharibiwa na matakwa yake yanayodanganya, na kufanywa wapya katika mitazamo ya mawazo yenu, na kutwaa uwepo mpya wenu, ulioubwa kwa mfano wa Mungu.” Waefeso 4:22-24

HALI YETU YA KIROHO huonyesha mwitikio wetu kwa mapenzi. Hufanya kazi katika maisha yetu **kutuwezesha kuzaa matunda ya Roho Mtakatifu. Sisi huonyesha upendo na shukrani zetu Kwa Mungu kupitia imani na utiifu. Yote ni kuhusu uhusiano.**

Mchoro unaofuata unaashiria jinsi watu wengi wanavyotatanishwa.



Wengi husema mambo kama “mimi? Nataka kwenda mbinguni. Lakini ninapoangalia nilipo na ninapotaka kufika, naona ugumu, ni kama haiwezekani kamwe.” Ukweli ni kwamba tunapomwamini Kristo, kwa macho ya Mungu tunakamilishwa kwa asilimia mia moja. Tunakamilishwa daima kwa sababu ya nehema ya Mungu pamoja na uwepo wetu katika Kristo. Yeye hutusaidia kuwa zaidi kama Kristo.

“...Kwa kuwa kwa kafara moja tu, daima amewakamilisha wale ambao wamefanyika watakatifu.” Wahebrania 10:14

“Mungu alikuokoa kwa nehema yake ulipoamini na wewe huwezi kupokea sifa kwa jambo hili. Ni Zawadi kutoka kwa Mungu. Wokovu sio malipo ya kazi njema tuliyoifanya, na kwa hivyo hakuna afaaye kujigamba.” Waefeso 2:8-9

Imani hii yetu hutupa amani, raha tumaini na uhakika hadi mwisho wa maisha yetu, wakati wa kubadilishwa huku.

“ Na ninao uhakika kuwa Mungu aliyeanzisha kazi nzuri ndani yetu ataiendeleza na kuikamilisha hadi Kristo atakaporudi. .” Wafilipi 1:6

Je, Mungu atakamilisha kazi yake ndani yetu lini?

KUMALIZIA: Tunaokolewa kwa minajili ya uwepo wetu wala sio kwa hali yetu! Hiyo ni nehema ya Mungu!

Karibu kila wakati, dhana hii huelekeza swali lingine: ina maana kuwa sio muhimu kuwa mwema, kuwa hali yetu haina umuhimu wowote?

Jawabu lipatikanalo katika agano jipya ni kuwa.. **NDIYO, NI MUHIMU!**. Hatufai kuzitumia vibaya zawadi za Mungu.

Ishi maisha ya walio huru, iwapokuwa msiutumie uhuru wenu kama funikio la dhambi. Ishini kama watumishi wa Mungu.” I Petero 2:16

Mtume Paulo aliandika, “Simaanishi kusema kuwa mimi nimekamika. Bado sijyajua yale yote ninayopasa kuyajua, lakini

nnaendelea kwa bidii hadi siku ile ambapo nitakuwa kile ambacho Kristo ameniokoa kwa ajili yake na anachotaka niwe.” Wafilipi 3:12

Yesu ananipenda jinsi nilivyo, ila hana mpango kamwe wa kuniacha katika jinsi hii.

Shinikizo langu la zamani lilikuwa nionekane mwema ili niokolewe. Ikiwa nitayafanya niyafanyayo kwa kusudi nionekane mwema, basi ubinafsi na woga ndizo motisha wangu. Hapo nitakuwa wa kujitakia, kufunikia, kukataa na kulinganisha. Sitawahi kujua iwapo nimetenda ya kutosha. Hivi ndivyo imani ya mwanadamu inavyojaribu kututawala kwa njia ya hofu.

Kwa kushawishiwa na nehema na upendo wa Mungu natazamia kuwa kama Yesu ili kumtukua Mungu na kumwonyesha upendo wangu, shukrani yangu, na mwikio wangu wa wokovu na yote aliyonitendea. Ninafahamu hatuwezi kufanya ya kutosha ila yale ambayo ameshayatenda ndiyo yanayohitajika maishani mwangu ili nipate kuwa na uhusiano wa kudumu na yeye.

Kuimarisha uhusiano wangu mpya na Yesu ndilo shinikizo langu lipya. Bila uhusiano wangu na yesu, mimi ni dhaifu na wala sina nguvu yoyote.

(Yohana 15:5).

Safari ya Maisha NJE YA KRISTO

Maisha NJE Ya Kristo

- Kukumbana na mauti
- Kulaaniwa
 - Kufa ki roho
 - Kupotelea gizani
 - Asioweza kujisaidika

Tunapoiamini kafara ya Kristo, kutubu na kubatizwa, tunavuka toka katika mauti na kuingia kwenye uzima.
Yohana 5:24

Safari ya maisha NDANI ya Kristo

Sehemu hii nyeupe inayaashiria maisha yetu nadani ya Kristo. Inaonyesha sehemu na hali yetu.

“Kwa kuwa Yeye alituchagua hata kabla ya kuumbwa kwa ulimwengu, tuwe watakatifu na wenye haki mbele zake.”

Waefeso 1:4

Kwa sababu ya sehemu yetu ndani ya Kristo, tumekamilika kwa asilimia miambe za Mungu kwa maisha yetu yote. Tutakapokufa, Mungu ameshatutayarishia makao mbinguni. Na hilo, je?

“Nasi tungali tunabadilishwa na kuwa mfano wake.” *2 Wakorintho 3:18*

Kupitia ‘kubadilishwa’ kwetu, tunakuwa kile ambacho, machoni mwa Mungu, tushakuwa. Katika safari yetu, tunakumbana na tusingoyataraji, machungu na pia hali ngumu. Kuna milima ya kupanda, mabonde ya kupitia na mawimbi ya kukabili.

HALI yetu huashiria hali yetuya ki-roho. Imara au dhaifu. Safari ya kila mmoja ni tofauti, ila mwisho wake ni mmoja tu. Kubadilika kungali kunaendelea.

“Jitahidie ukamilifu.” *II Wakorintho 13:11*

Matendo kama ya Yesu.

Dhambi = “lipoteza alama”

Ndani ya Kristu, Mungu hazihesabu dhambi za wanadamu dhidi yao. *II Wakorintho 5:19*



Katika kurudi kwa pili kwa Yesu... Tuta: Fufuliwa (*Ufunuo 21*)

NA Tuta: Kamilishwa Komaa (*Wakolosai 3:1-4*)


MKRISTO AFANYEJE ANAPOTENDA DHAMBI?

Japo ni jambo la kuepokwa, tutatenda dhambi hata baada ya kuwa wakristo. (1Yohana 1:8).

Tungali tunajifunza, tunakomaa, kujaribu, na wakati mwingine tunafeli. Hii ni sehemu ya safari ya kubadilishwa.

Wengi wana dhana potovu kuhusu msamaha wa Mungu. Wanayo dhana inayoitwa “imani ya Kistari”.

Kuishi juu ya kistari-wokovu



Kila kitu huanzia vyema. Tunamkubali Yesu na tunaendelea kuinuliwa., lakini tunapotenda dhambi, tunafikiri na kuhisi ya kuwa tumeanguka chini ya kistari. Tunaomba, “Mungu nisamehe! Na kutamani tuwe juu ya kistari tena, angalau hadi tutakapo tenda dhambi tena. Kwa muda, wasiwasi unatuingia- “niko juu au chini?” Tunakosa amani na kuwa na hofu. Mungu hafanyi kazi jinsi hii!

Inatupasa kufanya nini tunapotenda dhambi? Ni dhahiri...

“Iwapo tutayakiri makosa yetu, yeye ni mwaminifu na mwenye haki, na atatusamehe na kutusafisha kabisa kutokana na uovu wote.”


1 Yohana 1:9

Kutubu sio kusema ‘samahani’ bali ni kukubali “nlilitenda”. Ni kusema kuwa tunakubaliana na Mungu kuwa tuliyoyatenda, ni dhambi na kubali lawama hiyo.

Ni kwa nini tunahitaji kutubu? Ni ili kuziweka njia za mawasiliano sawa ili tuweze kuendelea kukua katika uhusiano wetu na Yesu.

Adamu na Eva walijificha kutoka kwa Mungu walipotenda dhambi. Tunapojaribu kuzificha dhambi zetu kutoka kwake, tunamfungia nje. Tunamfungia roho zetu. Tunadhoofishwa na kuwa wepesi wa kuharibiwa na fikira na mienendo miovu.

Mungu



anataka tuwe karibu naye, tumwamini na tumpende. Yeye anatumgojea tutubu.

Kwenye sarakasi, tunamwona msanii wa nyaya

za juu akiyafanya mambo yake ya kustaajibisha. Neti salama humpa motisha wa kuwa hodari. Hataki kuanguka, lakini kuna salama hata iwapo ataanguka. Mungu anatuita ‘tuondoke’ na tumfuate katika maisha haya mapya kiajabu. Hatutaki kuanguka wala kumdhalilisha Mungu. Hata hivyo, kunayo salama yetu iwapo hilo litatokea. Nehema ya Mungu ndio neti salama yetu.

Na tusipotubu je?

“ Wale ninaowapenda, mimi huwakosoa. Kwa hivyo, kuweni wakweli na mtubu” Ufunuo 3:19

Mstari huo ni ahadi ya kupendwa na Mungu.

“Mababa zetu walituaadhibu kadri walivyoona inafaa, ila Mungu hutuaadhibu kwa manufaa yetu sisi, kusudi tushiriki katika utakatifu wake. Adhabu zote zinapofanywa, huonekana chungu. Hata hivyo, baadaye, hutoa mazao ya wema, na amani kwa wale waliofunzwa kwake.” Wahibranian 12:10-11

TOBA NI:

- Kukubali lawama au matokeo ya matendo yetu.
- Kukiri kwake Mungu kuwa tunakubali ya kwamba tulitenda dhambi
- Kuashiria lengo letu la kubadilika.
- Kumshukuru Mungu kwa msamaha wake
- Kujaribu kuyarekebisha mahusiano yangu yaliyo haribika.

Agano jipya halitufunzi kuwa tukiomba msamaha kila wakati..tunao tayari. Tulihihiwa!

Tuhahitaji kutubu dhambi zetu kila wakati, kumshukuru Mungu kwa msamaha wake, na tena kuchukua hatua za kuishi katika njia zake.

NIOMBE KALAMU!

“ Lakini iwapo tutatembea kwa mwanga, jinsi yeye alivyo ndani ya mwanga, tuwe nao ushirika na wengine, na damu ya Yesu mwanawe itatusafisha kutoka kwa kila dhambi.” 1 Yohana 1:7

Je, umeyaelewa mambo haya?

Unayo maswali yoyote? Unamjua yeyote anayehitaji uhusiano mpya na Mungu?

